

LBE 2009 – Migration

Episode 4: Asylum Seeker

Author: Marta Barroso

Editor: Thomas Mösch

Characters:

Voice 1: Narrator, female

Voice 2: male, official attitude

Inserts:

Bobby (English, 1 German): male, 33 yrs

Eddie (German, 1 take only): male, +/- 36 yrs

Jean Pierre (French, 1 take only): male, +/- 35 yrs

Intro:

Hujambo na karibu kwenye makala ya Noa Bongo Jenga Maisha Yako kuhusu Uhamiaji. Kwenye kipindi hiki utapata kumfahamu Bobby, kijana wa Kiafrika anaeishi hapa Ujerumani kwa miaka sita sasa. Alipofika hapa Ujerumani aliomba hifadhi. Kwa muda wote huo anasubiri kupewa kibali cha kumwezesha kufanya kazi. Je maisha ya mtu ambae maombi yake ya hifadhi yamekataliwa yako vipi? Jiunge nasi ili upate kujua zaidi.

1. SFX: Typing machine

2. O-Ton Bobby:

„My name is Bobby.“

3. SFX: Typing machine

4. O-Ton Bobby:

„I'm 33 years now.“

5. SFX: Typing machine

6. O-Ton Bobby:

„Mimi ni mzaliwa wa Ghana.“

7. SFX: Typing machine

8. O-Ton Bobby:

“niko hapa nchini Ujerumani tangu mwaka 2003.”

9. SFX: Typing machine

10. Voice 1:

Lazima iwe hivi au hata na zaidi, wakati ambapo Bobby alikamilisha yote kabla ya kupata kibali cha kuishi Ujerumani. Hayo yalitokea mwaka 2005, baada ya kijana huyo kuwemo humu nchini kwa miaka miwili.

11. O-Ton Bobby:

“ni wapi nilipokuwa Ulaya, hata sijui, (...) weupe ni weupe tu. (...) Kwa sababu kwa mara ya kwanza nilipokuwa Ulaya sikuweza kutambua kama hapa ni Ujerumani, au hapa ni Italia, Uholanzi au Uhispania mpaka nilipokuja kujua kuwa niko Ujerumani.”

12. Voice 2:

Kutoka mwaka 1987 hadi mwaka 1992 idadi ya watu walioomba hifadhi iliongezeka zaidi hapa nchini Ujerumani. Kwa hivyo mnamo tarehe 1 mwezi Julai mwaka 1993, mabadiliko makubwa katika sheria za kuomba hifadhi yalianza kutumika rasmi . Moja kati ya mabadiliko hayo ni kuhusu kuingia katika jamuhuri ya shirikisho la Ujerumani. Ni kwamba yeyote anaeingia kutoka nchi ya tatu ambayo iko salama hana haki ya kupewa hifadhi ya kisiasa. Hiyo ina maana kwamba , nchi zote za Umoja wa Ulaya, Norway, Uswisi pamoja na nchi nyinginezo zinahesabika kuwa ni nchi za tatu salama”.

13. SFX: Typing machine, fade under**14. Voice 1:**

Bobby alikuja na meli ya makontena. Hajui safari hiyo ilichukua muda gani. Hakumbuki kabisa. Mara tu alipofika Ulaya mtu mmoja alimchukua kwa gari hadi kaskazini mwa Ujerumani.

15. O-Ton Bobby:

“Yule mtu aliniambia kuwa hapa ni Hamburg! Kwa hivyo unaweza kutafuta unakokwenda. Muulize mwafrika yoyote iwapo unahitaji usaidizi. Mimi nimefanya kazi yangu. Sikujui na wala wewe hunijui’.”

16. SFX: Typing machine, fade under**17. Voice 1:**

Bobby anakumbuka kuwa alikaa katika mji wa Hamburg, kwa takriban miezi minane kutoka mwezi Oktoba mwaka 2003 hadi mwanzoni mwa msimu wa kiangazi wa mwaka 2004. Aliyaendesha maisha yake kwa kuomba fedha kutoka kwa wapita njia. Alitaka kuboresha maisha yake ndiposa akaondoka kutoka kwenye mji wa bandari wa Hamburg hadi mji wa Essen, mji wa viwanda ulio magharibi mwa Ujerumani. Lakini hata katika mji huo wa Essen hakukaa kwa muda mrefu. Hayo yote lakini yako kwenye kapu la sahu ni ya zamani tangu mwaka 2005. Tangu wakati huo anaishi katika mji wa Cologne.

18. SFX: Sweeping, piece of cloth in the water**19. O- Ton Bobby:**

“Mimi ni mfanya kazi mwenye bidii (...), lazima kufanya kazi na usifanye mchezo kwa kila unachokifanya. Kwa sababu ukicheza hutaweza kupata chakula. (...) nisipo fanya kazi ninakuwa kama mgonjwa.”

20. Voice 1:

Bobby anaishi kwenye nyumba maalum ya watu wanaoomba hifadhi nje ya mji wa Cologne. Kila mwenye kuishi hapo anawajibika kuitunza nyumba hiyo. Nyumba nzee ambamo watu kadhaa kutoka kila pembe ya dunia wanaishi.

21. Voice 1:

Wakati wengine wana jukumu la kuitunza bustani au jikoni. Kijana huyo kutoka Ghana anawajibika kusafisha ngazi za nyumba hiyo mara tatu kwa wiki. Hiyo ndiyo kazi pekee anayoruhusiwa kufanya kwa sasa.

22. SFX: Moving the bucket with foot

23. Voice 2:

Maombi yake ya kutaka hifadhi bila shaka hayatakubaliwa iwapo alitokea kwenye nchi ambayo haina migogoro iliyo miongoni mwa nchi za tatu salama. Kwa mujibu wa serikali ya Ujerumani, nchi salama mwombaji anakotoka ni nchi ambayo haina migogoro ya kisiasa, haina adhabu zinazokiuka haki za kibinadamu au haina vitendo kama hivyo, na Ghana ni mojawapo ya nchi hizo salama “Nchi salama ya mwombaji anakotoka”.

24. SFX: Typing machine, fade under

25. Voice 1:

Alipofika Cologne, Bobby alifuata maagizo ya mtu aliyemleta mjini Hamburg: alikutana na mtu anayetoka nchini mwake na akaenda kuishi nae. Kwa sasa hajui aliko mtu huyo.

26. O-Ton Bobby:

“Siku moja nilikuwa chumbani na polisi waliingia na kumtaka kila mtu ajitambulishe, waliniuliza ilipo passpoti yangu nikajibu sina!”. nilikamatwa. (...) Nilipatwa na mshangao jinsi watu wanavyoweza

kupelekwa jela, sijawahi kuiba, sijauwa wala sijafanya kitu chochote kibaya. Yaani kwa sababu ya karatasi tu, nilishtuka sana.”

27. SFX: Typing machine, fade under

28. Voice 1:

Maofisa walimuhoji kila baada ya wiki mbili alipokuwa jela. Alizuiliwa kwa muda wa miezi minane. Baada ya kuachiwa alipata kibali cha “kuvumiliwa”.

29. Voice 2:

Kifungu cha 16a cha katiba ya Ujerumani kinawahusu watu wanaoandamwa kisiasa. Hawa ni watu ambao kutokana na rangi, dini, uraia kuwa wafuasi wa kundi au itikadi ya kisiasa ya kundi fulani, watu ambao wameathirika kutokana na kuandamwa na serikali zao au wanakabiliwa na hatari ya kuandamwa hadi kufikia wakati wa kuondoka kwenye nchi zao. Maombi ya watu wa aina hiyo yakikataliwa basi mtu huyo atapewa kibali cha “kuvumiliwa” na Jamuhuri ya Shirikisho la Ujerumani hadi pale serikali itakapoamua kumrudisha mtu huyo kwao. Kibali hicho kinaitwa – “Duldung” kwa lugha ya Kijerumani – mtu akiwa na kibali cha aina hiyo, anaweza kurudishwa kwao mara moja au pia anaweza kubakia nchini Ujeruamni kwa miaka kadhaa.

30. O-Ton Bobby:

“Duldung (kuvumiliwa) ni kama vile unaregarega, sawa na kuwa mguu mmoja uko ndani ya gari na mwingine uko nje. Chochote chaweza kutokea: ni uwe unaendesha gari yako mwenyewe la sivyo gari nyingine itakuja na kukuchukua.”

31. SFX: Typing machine, fade under

32. Voice 1:

Bobby ni fundi wa magari – hiyo ndio kazi yake na pia ni zawadi kwake, anasema. Hakupata hifadhi, ombi lake lilikataliwa kwa sababu waliomwandama hawakuwa maafisa wa serikali au watu walio kuwa karibu sana na serikali..

33. O-Ton Bobby:

“Kuna mtu aliwatuma watu kuja kuniuwa. Kwa sababu biashara yangu ilikuwa inakwenda vizuri na yake haikuwa ikienda vizuri, kwa hivyo alijaribu kunishambulia . (...) Kila nilipopata simu zilikuwa za vitisho, niliambiwa kuwa nikirudi nitauwawa!”, kwa hivyo niliona maisha ni mahala popote. Nilisema popote pale naweza kupata utulivu. (...) Lakini kwa vile hakuna usalama – nilijua kuwa maisha yangu yako hatarini, nililazimika kuondoka nchini .”

34. SFX: Typing machine, fade under

35. Voice 1:

Bobby alikuwa nje kwenye karakana yake wakati mwenziwe alipompigia simu kumuonya. Hakurudi tena. Mjomba wake alimtayarishia kila kitu. Aliishi kwake na yeye ndie aliyegharamia safari hiyo mpaka siku ya kusafiri. Kutoka wakati huo – na katika miaka yote hii ya kusubiri – Bobby amejifunza kuwa mtulivu maishani.

36. O-Ton Bobby:

“Sijui Mungu amenipangia nini, lakini mimi kila nikiwaza kurudi naona kama kila kitu kitakuwa sawa tu, Mungu atanionyesha kama kukaa hapa ndio vizuri kwangu, basi Mungu atanisaidia nitaishi hapa, na ndio maana niko hapa. Lakini sijui ya kesho au ya keshokutwa. Kwa hivyo (...) ninasubiri Mungu ajibu maombi yangu.”

37. Voice 2:

Mwaka 2008, takriban watu 22,000 waliomba hifadhi nchini Ujerumani. Maombi 3,856 yalipokelewa kutoka Afrika kabla mwaka uliotangulia. Maombi mengi kutoka Afrika yalikuwa ni ya watu kutoka Nigeria, wakifuatiwa na watu kutoka Algeria na Eritrea. Ghana ilikuwa nafasi ya nne ni watu 206 walioomba hifadhi.

38. Music “No woman no cry”, then fade under

39. SFX: Typing machine, fade under

40. Voice 1:

Hali ya hewa inapokuwa nzuri, Bobby anapenda kukaa muda mrefu nje, mbele ya nyumba. Kukinyesha au theluji inapodondoka basi yeye hukaa tu ndani ya chumba chake – kwa kawaida anapenda kusikiliza muziki.

41. O-Ton Bobby:

“Wakati wote huwa nafikiria na kufikiria, mawazo sio mazuri kwangu. Sijisikii vizuri moyoni mwangu. (...) Muziki ninaousikiliza ni muziki unaonipa matumaini, unanipa furaha na unanipa maisha.”

42. SFX: Bobby singing “No woman no cry”, then fade under

43. Voice 1:

Chumba chake kina upana wa mita kumi na mbili mraba, kimejaa vitu. Kuna mabegi ya kusafiria yenye nguo zinazoning’inia. Viatu vya kila rangi tena vya kila msimu vimetupika tupika kila mahali kwenye sakafu. Makoti yananing’inia moja juu ya jingine kwenye misumari ya mlangoni . Lakini vitu hivi au vingi kati ya vitu hivyo sio vya Bobby. Ni vya rafiki aliyekutana nae kwenye timu ya mpira ya waafrika ya hapo mjini.

44. O-Ton Jean-Pierre_12, french:

Sidhani – najua kuwa yeye ni mtu mzuri. Kwa sababu nimemfahamu kwa muda mrefu, tangu nilipokuwa na kampuni yangu hapa na anafanya kazi vizuri. Yeye ni rafiki yangu, kwa hiyo ana haki ya kuja kwenye kampuni yangu. Lakini kunisaidia tu, sio kupata mshahara .“

45. Voice 1:

Haijulikani iwapo anapata pesa kutoka kwa rafiki yake au la. Lakini kama mfanya usafi katika nyumba ya wakimbizi: Si rahisi kwa Bobby kuingia kwenye matatizo. Leo ni Jumapili na kwa Bobby ni wakati wa kwenda kanisani.

46. SFX: Bobby talking to his friend:

...Ok, tutaonana baadaye ok kwaheri!

47. SFX: Bobby leaving his room and closing the door

48. SFX: Footsteps leaving the house, fade under

49. Voice 1:

Jumapili ni siku muhimu sana kwa Bobby. Kwa ajili ya misa amefumua nywele zake alizokuwa amesuka – alikuwa ameziacha hivyo kwa muda wa wiki kadhaa – amevaa suti nyeusi na shati jeupe. Na mkononi amebeba mfuko wa plastiki na ndani yake kuna biblia na sufuria safi. Anataka kurudisha sufuria hiyo kwa mwanamke aliyemtayarishia chakula cha Kiafrika wiki iliyopita .

50. O-Ton Bobby:

“Ninamuita Mama, Mama. Kwa hivyo ananiita mimi mtoto: ‘Leo ninataka kukupa kitu cha kula.’ Ndivyo alivyonipa chakula hiki.”

51. SFX: Typing machine, fade under

52. Voice 1:

Mama pia anakwenda kwenye kanisa la Pentecosti lililopo vituo vichache vya basi kutoka nyumbani kwa Bobby. Misa hufanyika kwenye ukumbi wa utamaduni saa nane na nusu mchana kila siku ya jumapili. Ndio maana Mama anaelewa kuwa Bobby anatamani chakula cha Kiafrika kama vile.

53. O-Ton Bobby:

“Mna vyakula vingi hapa. (...) mna fu-fu, na sisi tuna tunakula fu-fu tofauti , sio kama viazi. Sio kabisa. Ngoja nikwambie, fu-fu ya muhogo, fu-fu ya ndizi, fu-fu ya viazi vikuu, zote zinapatikana hapa, ni ghali mno. Kwa hivyo ni lazima ule vyakula vya Kijerumani. Mara nyingine havina ladha. Lakini kutokana na hali yako inabidi ujilazimishe kula vyakula hivyo. Hata ingawa saa nyingine unakumbuka chakula, mama yako alichokuwa akikupikia.”

54. SFX: Typing machine, fade under**55. Voice 1:**

Huku Bobby akiwa anasubiri uamuzi wa idara kuu ya uhamiaji na maswala ya wakimbizi iwapo ataruhusiwa kukaa au itambidi kuondoka kutoka humu nchini, anaishi tu siku hadi siku bila kujua hasa muelekeo wa maisha yake ni upi. Anaendelea kufanya kazi, au kusubiri, anapanda basi moja au treni, na Wajerumani, anakwenda kwenye maduka ya chakula pamoja na Wajerumani hao hadi siku ile atakapo pata kibali chake cha kufanya kazi kutoka kwa ofisi zinazohusika. Ndipo hapo atakapokuwa kwamba miguu yake yote miwili imo ndani ya gari lake ama la

56. O-Ton Bobby:

“Hadithi yangu imeishia hapo!”

57. SFX: Typing machine, suddenly stops**Outro:**

Bobby alimweleza Marta Barroso hadithi yake hiyo. Na hapo ndio tumekamilisha makala ya leo katika Noa Bongo Jenga Maisha Yako kuhusu uhamiaji. Iwapo unataka kujifahamisha zaidi juu ya maswala ya uhamiaji ya nchini Ujerumani, tembelea mtandao wa idara kuu ya Uhamiaji na maswala ya wakimbizi. Anuani yao ni: www.bamf.de Kumbuka unaweza kukisikiliza tena kipindi hiki au kipindi kingine chochote cha Noa Bongo jenga Maisha Yako kwenye mtandao, anuani yetu ni: www.dw-world.de/lbe Usikose kujiunga nasi tena kwenye kipindi kijacho. Kwaheri.